

## WAZAZI WANA WAJIBU WA KUFANYA KILA JUHUDI ILI KWALINDA BINTI ZAO

Je, unapaswa kuwasiliana na nani iwapo  
hatari itatoka?

### NG'AMBO?

- Kamati ya Mataifa ndani ya Afrika kuhusu Shughuli za Kitamaduni: <http://www.iac-ciaf.net>
- Orodha ya Balozi za Ubelgiji ng'ambo:  
<http://diplomatie.belgium.be>

### NCHINI UBELGIJI?

- Au nambari za bila malipo: 1712 kwa wahusika ambao wanataka kutoa malalamishi kuhusu ghasia au unyanyasajji (Jumuiya ya Kiflemi) au 103 Ecoute Enfants (Jumuiya ya Ufaransa)
- INTACT: +32 (0)499 83 29 42

Kwa maelezo yote kuhusu FGM, tafadhali wasiliana na mashirika yafuatayo:


- GAMS Belgique: +32 (0)2 219 43 40 - [www.gams.be](http://www.gams.be)
- INTACT: +32 (0)499 83 29 42 - [www.intact-association.org](http://www.intact-association.org)
- Le Centre de Planning Familial des FPS de Liège:  
+32 (0)4 223 13 73 - [www.planningsfps.be](http://www.planningsfps.be)



SWAHILI

## SHERIA ZA UBELGIJI ZIMEPIGANA MARUFUKU

ukeketaji wa wanawake  
hana na ambo



Federal Public Service  
Justice



KINGDOM OF BELGIUM  
Federal Public Service  
Foreign Affairs,  
Foreign Trade and  
Development Cooperation



federal public service  
HEALTH, FOOD CHAIN SAFETY  
AND ENVIRONMENT

## JE, UKEKETAJI WA WANAWAKE (FGM) NI NINI?

Hii ni kuondolewa sehemu kiasi au sehemu yote ya jenitelia kwa sababu zisizo za matibabu.

### KWA NINI UWE NA HATI HII?

Hati hii inakuruhusu kuelezea familia yako kuwa FGM imepigwa marufuku katika Ubelgiji na unaweza kufungwa jela kwa kumkeketa binti yako, hata iwapo hii ilifanyikia ng'ambo.

**Tafadhali jisikie huru kuhifadhi hati hii unaposafiri ili  
uionyeshe familia yako iwapo unashnikizwa kufuata mila hii.**

### AFYA YA WASICHANA WACHANAGA NA WANAWAKE

FGM ina athari kubwa ya kiafya kwa wasichana na wanawake.

Baadhi ya madhara yanaweza kutokea mara moja, kama vile kupoteza damu na/au maambukizi hatari, yanayoweza kusababisha kifo. Madhara mengine yanaweza kutokea baadaye: maumivu wakati wa hedhi, maambukizi katika sehemu za uzazi yanayoweza kusababisha utasa, maumivu wakati wa kushiriki ngono, matatizo sugu ya mkojo, matatizo wakati wa kujifungua, lakini pia wasiwasi na ungogovu.

## SHERIA INAPIGA MARUFUKU FGM

Sheria za kimataifa zinazingatia ukeketaji wa wasichana na wanawake kuwa ukatili na udhalilishaji ambao ni sawa na mateso. Kila mmoja ana haki ya kuwa na uadilifu wa kimwili na kiakili.

### Ulimwenguni?

Itifaki ya Maputo (2003) barani Afrika inahitaji kuwa majimbo yapige marufuku aina zote za FGM, kwa hatua za kisheria na vikwazo. Nchini Senegali, Burkina Faso, Togo na Kodivaa shughuli hii imepigwa marufuku kisheria.

### Na nchi ni Ubelgiji?

FGM pia imepigwa marufuku na Sheria za Ubelgiji na inazingatiwa kuwa unyanyasaji.

Kifungo cha miaka 3 hadi 5 katika jela kwa "yejote ambaye ameshiriki, amechangia au amehimiza aina yoyote ya ukeketaji wa mtu yeyote wa kike, au amejaribu kufanya hivyo, na au bila ridhaa yake". Iwapo ukeketaji unatekelezwa kwa msichana wa chini ya umri wa miaka 18, kifungo kinaweza kuwa kikubwa. Sio tu mwandishi pekee wa ukeketaji anawenza kushtakiwa au kuadhibiwa nchini Ubelgiji, pia mshirika anawenza kushtakiwa na kuadhibiwa. (art. 409 Kanuni ya Adhabu Ubelgiji)

Hii inamaanisha kuwa wazazi wanaweza kushtakiwa nchini Ubelgiji iwapo binti yao amekeketewa ng'ambo. (art. 10 ter CICr).